

Lugha, uwezo na msaada madhubuti

Ellie Kemp, Mkuu wa Mwitikio wa Mikasa, Translators without Borders

Nini kilichoko katika neno? Suala kubwa, wakati mwingine.

Kwa Mkimbizi mmoja Ugiriki, hapakuwa na maneno ya kuelezea ugonjwa wake kwa sababu hapakuwa na wakalimani waliopolekwa hospitalini alipokuwepo; Alikuwa na kiwewe ambacho kilisababisha hali mbaya ya umbumburushaji. Kwa kikundi cha wanawake huko Bangladeshi, hali ya kutoweza kusoma maelekezo ilisababisha taulo za hedhi ambazo zilitolewa katika mpango wa mwitikio wa mikasa kutoeleweka na kuonekana hazina maana. Kwa mkimbizi mmoja aliyerudishwa Nigeria ya kaskazini alipokua anaomba ushauri kujua haki zake, ukosefu wa lugha ya pamoja na wanasheria ulimnyima uhuru wake, na kumfanya antegemee mtu mwingine kutoka jamii ya wenyeji kumtafsiria lugha hiyo.



Mama na mtoto wanalala baada ya kuwasili Lesvos, Ugiriki kwa kutumia boti' - (c) Karim Ani.

Kwa wanaopatwa na mikasa, neno kwenye lugha sahihi, ama neno ambalo husemwa wakati maandiko hayaeleweki lina uwezo wa kuleta huduma, heshima na haki za binadamu.

Katika sekta ya kibinadamu, mara nyingi hatuna uhakika kuwa tunawasiliana na waathirika kwa lugha na njia ambayo wanaielewa. Suala hilo hujitokeza hasa katika mazingira yahusishayo mchipuko wa mikasa au kwa waathirika wanaoongea lugha au lahaja tofauti.

Kwa nini lugha ni changamoto kwa mwitikio wa misaada ya kibinadamu

Jambo moja ni **ukosefu wa taarifa**: katika mazingira tofauti kilugha, takwimu za kawaida juu ya lugha na masuala ya mawasiliano kwa idadi ya waathirika hazichukuliwi kwa utaratibu maalumu na kutolewa kwa namna ambayo barabara hutumiwa au maeneo ambayo huweza kuwa na vizuizi barabarani. Hivyo basi, kutokuwepo kwa takwimu dhairi kunasababisha tufanye makadirio: kwamba watu wanaoongea lahaja tofauti huelewana, au taarifa hiyo inapokelewa sawa kwa wanaume na kwa wanawake.

Uhitaji wa **kasi** unaweza kuzuia mawasiliano madhubuti, hususan katika dharura za ghafla. Wakusanyaji wa takwimu kama vile Ushahidi na QCRI huweza kupata na kueneza kwa haraka jumbe zilizobainishwa kimaeneo kutoka kwa watu walio katika hali ya mtanziko kutokana na majanga ili kusaidia kuelekeza juhudi za mwitikio wa mikasa – ila kama jumbe hizo haziko katika mfumo wa lugha wa ‘kimataifa’ mara nyingi haziezi kuendelezwa.

Kwa kawaida **mfumo wa uongozi wa juu-chini** wa kutoa msaada hauwezi kusaidia. Mwitikio wa msaada wa kibinadamu hutekelezwa na wataalamu wa kimataifa na hata kitaifa katika lugha ya kimataifa au ya kitaifa. Ni rahisi kukosa vipingamizi vya lugha ambavyo huwatenga wengine kwa mahojiano.



‘Wanaume wanazungumza wilayani Yabo, kaskazini mwa Nijeria’ - © 2002 Kituo cha Mawasiliano ya Miradi, kwa ustahiki wa Photoshare.

Matatizo haya huunda **mfumo wa masuala pamoja na lugha**: watu wanaozungumza lugha za ‘wachache’ hutengwa kwa njia zingine pia. Kama siongei lugha rasmi ya taifa, yawezakua sikuendelea sana katika masomo. Labda siwezi kusoma vizuri, na vipeperushi vya msaada ni

kama karatasi za rangi tu kwangu; Pia ni vigumu kwangu kuja kutoa maoni yangu au kusema ninachohitaji.

Katika maeneo mengine, ufahamu wa lugha ya mama unaweza kukufahamisha kiasi juu ya kipato cha familia yangu, hali ya lishe langu na uwezekano wangu wa kuolewa katika umri wa miaka 12. Lugha inaweza kuwa msaada kwa mazingira magumu – ikiwa kama unaweza kuepukia mahali palipo na usalama wakati wa mapigano, au mazao yako kustawi wakati wa ukame, au nyumba yako kustahimili tetemeko la ardhi.

Kwa maneno mengine, mara nyingi wale watu ambao mashirika ya kibinadamu wanataka kusaidia ndio huwa vigumu kuwasilana nao.

Kukabiliana na changamoto: mawasiliano kwenye lugha sahihi

Translators without Borders hutoa huduma za lugha kusaidia kutatua changamoto hizo. Kutokana na msaada wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi kupitia Fedha za Ubunifu wa Jamii, tunaendeleza uwezo wa mwitikio wa mikasa kupitia mpango wa Words of Relief kwa zaidi ya miaka miwili ijayo, ili:

Kuendeleza ufahamu wa masuala ya lugha na mawasiliano katika juhudi za utoaji wa msaada, kusaidia muundo wa huduma kama vile ushauri wa faragha. Tutashirikiana na wengine tupate takwimu za lugha zinazozungumzwa, kiwango cha ufahamu na njia za mawasiliano katika mazingira maalumu ya dharura, ili kusaidia mipango ya utoaji msaada. Tutaendelea kwa ukusanyaji wa takwimu juu ya masuala hayo, na kusaidia mashirika kujua ni kwa namna gani idadi husika inaelewa vifaa vilivyopo.

Kuongeza usaidizi wa lugha kwenye nchi zilizoathiriwa na vita, kwa hiyo kuna mkalimani tayari wakati kwa mfano mkimbizi anapohitaji huduma hiyo. Tutaongeza huduma za tafsiri kwa wengi, kuwapatia mafunzo watoa misaada wakalimani na watafsiri, na usaidizi mwingine wa istilahi kuboresha usawa. Tutaunda vikundi vya kutoa tafsiri ya mawasiliano ya dharura kwa haraka panapotokea dharura, tukishirikiana na wakusanyaji takwimu kuhakikisha kuwa taarifa za lugha chanzi hazipotei. Kwa lugha zilizo na wataalamu wachache waliofuzu, tutawekeza zaidi katika mafunzo, usaidizi na uhakiki ubora ili kuongeza uwezo kwa siku za usoni.

Kuijenga lugha kwenye utayari, kwa kuhifadhi vifaa kwenye lugha za nchi zilizoathiriwa zaidi na vita, kusaidia kuhakikisha kuwa hakuna msaada ambao haupewi kipaumbele kwa ukosefu wa ufahamu. Tutatumia na kuendeleza teknolojia ya maendeleo kama vile utafsiri wa mashine, kumbukumbu za tafsiri na aplikesheni za simu kuongeza kasi, unadhifu na uwezo wa kufikisha mawasiliano kwenye lugha husika.

Wakimbizi, wakimbizi wa ndani na wanawake ambao mazao yao yameharibiwa wote watapata msaada wa lugha kutoka kwa watoa misaada. Tunatarajia kwamba tutasaidia kuiwezesha hii.



Wanawake wako mtoni kule Kustiya, Bangladesh wakifua' - © 2014 Momo Mustafa kwa ustahiki wa Photoshare.



Ministry of Foreign Affairs



Humanitarian
innovation fund

elrha